# UTEKELEZAJI WA AFUA YA UANGAMIZAJI WA VILUWILUWI WA MBU(LARVICIDING) WAENEZAO MALARIA

## Kikao cha waganga wakuu wa Mikoa na Wilaya
## Ukumbi wa LAPF
## DODOMA 13-18/08/2018

# YALIYOMO

- Utangulizi
- Malengo ya Udhibiti wa Malaria.
- Utekelezaji wa Afua ya “Larviciding”
- Ulipaji wa gharama za viuadudu.
- Fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Afua ya “Larviciding”
- Changamoto za utekelezaji wa afua ya Larviciding
- Mambo yanayotakiwa kufanyika katika Mikoa na Halmashauri
- Hitimisho.

# UTANGULIZI

- Afua ya larviciding ni moja ya mkakati muhimu katika udhibiti wa mbu (Malaria vector control). Afua hii huangamiza viluwiluwi wa mbu katika mazalia katika hatua ya awali (larva stage).

- Serikali kwa kutambua umuhimu wa Afua hii katika udhibiti wa malaria nchini, imejenga Kiwanda cha Viuadudu Kibaha Mkoani Pwani kwa kutumia fedha zake yenyewe kwa asilimia 100.

# UTANGULIZI…

- Katika kuhakikisha azma ya Serikali inafanikiwa, mnamo tarehe 22 Juni, 2017 Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa agizo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kununua viuadudu na kutumia kwa ajili ya kuangamiza viluwiluwi wa mbu kwenye mazalia.

- OR-TAMISEMI ikiwa na jukumu la kusimamia Mikoa na Halmashauri, imeweza kuratibu ununuzi na matumizi ya viuadudu kutoka kiwandani ambapo mikoa yote 26 na Halmashauri 184 (100%) nchini zimeshachukua viuadudu na kuanza zoezi la upuliziaji katika maeneo yenye mazalia ya mbu.

# LENGO KUU

**Lengo Kuu: Kupunguza kiwango cha maambukizi ya malaria kitaifa kutoka wastani wa asilimia 10 % kwa mwaka 2012 hadi chini ya asilimia 1 % ifikapo Disemba 2020.**

**Mikakati Mikuu:** Mikakati iliyowekwa ili kufikia Lengo itajikita katika maeneo yafuatayo :

- maambukizi ya malaria kwa kuinua na kuendeleza Afua za kudhibiti mbu waenezao malaria
- Kuzuia ongezeko la wagonjwa na vifo vitokanavyo na malaria kwa kuzingatia upimaji na utoaji tiba sahihi mapema
- Kuhamasisha jamii kuhusu mabadiliko ya tabia chanya juu ya matumizi ya afua za kudhibiti malaria
- Kuhakikisha usimamizi thabiti na matumizi sahihi ya rasilimali fedha za shughuli za kudhibiti malaria



# Mikakati ya udhibiti wa malaria

### 1. UDHIBITI WA MBU KWA UTANGAMANO

- VYANDARUA VYENYE DAWA
- UPULIZIAJI VIUATILIFU UKOKO
- UANGAMIZAJI VILUILUI
  - VIUADUDU
  - UDHIBITI WA MAZINGIRA

### 3. UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI

- UFUATILIAJI & HATUA STAHIKI
- KUZUIA MATUKIO YA MILIPUKO
- UFUATILIAJI MAHSUSI WA WAGONJWA ili kutokomeza malaria)

### 2. UPIMAJI NA TIBA SAHIHI YA MALARIA PAMOJA NA TIBA KINGA

- UPIMAJI
- MATIBABU SAHIHI
- TIBA KINGA
- USAMBAZAJI
- WAKATI WA DHARULA

**MAWASILIANO KUHUSU MABADILIKO YA TABIA**

**UENDESHAJI BORA WA MPANGO, URATIBU WA WADAU NA RASILIMALI FEDHA**

**UIMARISHAJI WA MIFUMO YA UENDESHAJI SEKTA YA AFYA**

# Viashiria muhimu vya malaria


**Matokeo (outcomes):**


•**Matukio ya wagonjwa wa malaria** (kwa mujibu wa takwimu za vituo vya kutolea huduma) yamepungua kwa takriban **62%** kutoka  wahonjwa 295/1000 watu (2008) hadi wagonjwa 112/1000 watu (2017);

•**Idadi ya vifo kutokana na malaria imepungua kwa 73%** kutoka vifo 33/1000 watu (2008) hadi vifo 9/1000 (2017);

•**K**
20

•Id
**im**
ma





# UTEKELEZAJI WA AFUA YA “LARVICIDING’’

- Hadi kufikia mwezi Julai 2018, Mikoa na Halmashauri ilichukua viuadudu kwa awamu mbili,
  - Awamu ya kwanza, jumla ya Mikoa 14 iliyokuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya malaria (High Malaria Prevalence)
  - Awamu ya pili ni Mikoa 12 yenye kiwango kidogo cha malaria(Low Malaria Prevalence)
- Halmashauri 179 kati ya 185 (97%) zimeweza kutambua maeneo ya mazalia ya mbu katika maeneo yao.

# Kiasi cha viuadudu kilichopokelewa



# Matumizi ya Viuadudu…



# Zoezi la upuliziaji Viuadudu Mkoani Katavi



# Zoezi la upuliziaji Viuadudu Mkoani Shinyanga



# HALI HALISI YA ULIPAJI WA DENI LA VIUADUDU KIWANDANI BIOTECH-KIBAHA HADI KUFIKIA JULAI 27, 2018


- Hadi kufikia Julai 27, 2018 kiasi cha shilingi 307,422,884 kati ya 1,760,880,000 kimeweza kulipwa kwa ajili ya kulipia gharama za viuadudu vilivyochukuliwa toka Kiwandani Kibaha, sawa na asilimia 18 tu.

- Halmashauri 32 (40%) kati ya Hamashauri 80 zilizopo katika mikoa 12 ikiwemo na Halmashauri moja Mkoani Simiyu (Bariadi TC) zimeweza kulipia deni kiwandani.


# ULIPAJI WA DENI LA VIUADUDU

- Mikoa 5 kati ya mikoa 13 inayodaiwa gharama za viuadudu imeweza kulipa deni hilo kiwandani, ambayo
  - Arusha (Halmashauri 1),
  - Kilimanjaro (Halmashauri 4),
  - Dar es Salaam (Halmashauri 1),
  - Songwe (Halmashauri 1),
  - Njombe (Halmashauri 1) na
  - Rukwa (Halmashauri 2).


# Mchanganuo wa Deni la Viuadudu Kimkoa



# Mchanganuo wa kiasi kilicholipwa



# Bakaa ya Deni la Viuadudu



# MIKOA ILIYOTENGA FEDHA KWA MWAKA 2018/19

- Jumla ya fedha Tshs 8,982,310,817 zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi na matumizi ya Viuadudu kwa Halmashauri 179 Nchini.

- Halmashauri tano hazijawasilisha Bajeti kwa ajili ya ununuzi na matumizi ya viuadudu;

-Tabora(Urambo DC na Uyui DC)

-Mtwara(Mtwara MC )

-Lindi (Lindi MC)

-Arusha(Ngorongoro DC)

# CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA LARVICIDING

- Asilimia 90 ya Halmashauri zote nchini kutotenga fedha kwa 2016/17 na 2017/18 kinyume na maelekezo yaliyotolewa na OR-TAMISEMI mwaka 2016 hivyo kusababisha ugumu katika eneo la gharama za uendeshaji ikiwa ni pamoja na ulipaji wa Deni Kiwandani.

- Mtazamo hasi wa baadhi ya wakurugenzi katika mikoa 12 ya awamu ya pili kuhusiana na ulipaji wa gharama za ununuzi na matumizi ya viuadudu,hivyo kupelekea kasi ndogo ya ulipaji wa deni.

- Kukosa utaalamu wa kutosha na vifaa kwa ajili ya zoezi la ufuatiliaji (scooping) katika baadhi ya Halmashauri

# MIKAKATI YA SERIKALI

- Kuhakikisha Halmashauri zinatenga fedha katika Mipango na Bajeti  kwa kila mwaka mpya wa fedha,kwa ajili ya kutekeleza afua ya Larviciding.

- Wizara ya Afya maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto  pamoja na OR-TAMISEMI kuwashirikisha wadau wa maendeleo katika kuandaa kitita cha Uraghibishi kwa lengo la kutafuta fedha zaidi ili kusaidia Mikoa na Halmashauri kutekeleza afua ya ‘’Larviciding’’ na ‘’Indoor residual Spraying’’

# Mikakati ya Serikali

-Njia hizo zimeonekana kukosa wadau wakusaidia ukilinganisha na ugawaji wa vyandarua au upatikanaji wa dawa kwa ajili ya matibabu ya malaria.

- Kuhakikisha Halmashauri zinatenga fedha katika Mipango na Bajeti  kwa kila mwaka mpya wa fedha,kwa ajili ya kutekeleza afua ya Larviciding.

# Mikakati ya Serikali

- Wadau wameelekezwa kuwasilisha mipango yao OR -TAMISEMI ili ifanyiwe mapitio kabla ya utekelezaji ili ifuate vipaumbele vya serikali ambapo kwa sasa kipaumbele kimojawapo katika eneo la kupambana na Malaria ni kuwekeza katika afua ya “Larviciding” katika kuangamiza mazalia ya Mbu waenezao malaria.

- Kusimamia Halmashauri zote ambazo hazijalipa Deni la gharama za Viuadudu ziweze kulipa
- Wizara ya Afya kupitia NMCP kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inaendelea na zoezi la ufuatiliaji wa mbu wapevu(Entomological surveillance) katika maeneo yenye Kiwango kikubwa cha Maambukizi ya Malaria pamoja na Ufuatiliaji wa Matumizi ya Malaria Dash board na MSDQI katika kuboresha takwimu za malaria,kugundua tatizo mapema na kutafuta ufumbuzi

# Mikakati ya Serikali

- Wadau wameelekezwa kuwasilisha mipango yao OR -TAMISEMI ili ifanyiwe mapitio kabla ya utekelezaji ili ifuate vipaumbele vya serikali ambapo kwa sasa kipaumbele kimojawapo katika eneo la kupambana na Malaria ni kuwekeza katika afua ya “Larviciding” katika kuangamiza mazalia ya Mbu waenezao malaria.

- Kusimamia Halmashauri zote ambazo hazijalipa Deni la gharama za Viuadudu ziweze kulipa
- Wizara ya Afya kupitia NMCP kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inaendelea na zoezi la ufuatiliaji wa mbu wapevu(Entomological surveillance) katika maeneo yenye Kiwango kikubwa cha Maambukizi ya Malaria pamoja na Ufuatiliaji wa Matumizi ya Malaria Dash board na MSDQI katika kuboresha takwimu za malaria,kugundua tatizo mapema na kutafuta ufumbuzi

# Mambo yanayotakiwa kufanyika katika Mikoa na Halmashauri

- Kutambua mazalia halisi ya mbu kwa kuwatumia wataalamu wa masuala ya Vector Control
- Kufanya upuliziaji kwa vipindi sahihi (upuliziaji usifanyike kipindi cha mvua).
- Kufanya ufuatiliaji wa kupungua kwa mbu katika mazalia kwa vipindi sahihi kulingana na Miongozo iliyotolewa
- Kutoa Taarifa ya utekelezaji kwa wakati siku ya 14 kila baada ya robo(Quarterly).
- Kulipa Deni kwa wakati,ili Kiwanda kiweze kuendelea na uzalishaji.

# Hitimisho

Kwa kuwa ili kupambana na Malaria afua zaidi ya moja inatakiwa kutumika .

Afua hizo ni

- Indoor Residual Spraying”Matumizi ya vyandarua,Usafi wa mazingira na ufukiaji wa mashimo maeneo ya migodi au maeneo ambayo uchimbaji wa mchanga unaendelea

- Uchunguzi(Diagnosis) na Matibabu (Treatment) sahihi ya wagonjwa wa ndani(Inpatient) na nje(Outpatient) ambao wamegunduliwa kuwa na Malaria ni jambo la kuzingatia ili kupambana na Ugonjwa wa Malaria.

# Hitimisho

- Afua zilizotajwa zinatakiwa ziende sambamba na “Larviciding”kwani kuacha njia mojawapo miongoni mwa zilizotajwa inaweza kupelekea tatizo la ugonjwa wa Malaria miongoni mwa jamii kujirudia au kiwango cha maambukizi kuongezeka.

- Halmashauri zinatakiwa kulipa deni ili kiwanda kiendelee na uzalishaji kwa manufaa ya Taifa.

# Asanteni kwa Kunisikiliza